***Notisi ya Faragha:*** **Tarehe ya Kuanza Kutumika: Machi 26, 2013; Tarehe ya Marekebisho: Februari 1, 2026**

NOTISI HII INAELEZEA JINSI MAELEZO YAKO YA KIAFYA YANAWEZA KUTUMIKA NA KUFICHULIWA NA JINSI UNAVYOWEZA KUFIKIA MAELEZO HAYA. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI.

Notisi hii inaelezea desturi za faragha za vitengo husika vya Walmart vinavyochakata maelezo ya kiafya. Vitengo husika vinavyochakata maelezo ya kiafya ni pamoja na duka la dawa na huduma za macho za Walmart Health & Wellness, Sam's Club Health & Wellness, na huduma za Walmart Healthcare Research Institute. Tunaelewa kuwa maelezo yako ya afya ni ya kibinafsi na tunajitahidi kuyalinda. Tunahitajika kisheria kudumisha faragha ya maelezo yako ya kiafya yanayolindwa ("PHI"), kukupa Notisi hii ya majukumu yetu ya kisheria na shughuli za faragha zinazohusiana na PHI yako, na kukuarifu kuhusu ukiukaji wowote wa usalama unaohusisha PHI yako isiyolindwa. Sharti tuzingatie masharti ya Notisi ya sasa.

**Matumizi na Ufichuzi wa PHI Usiohitaji Idhini Yako: 1. Kwa Matibabu.** Tunaweza kutumia na kufichua PHI yako kwa madhumuni ya matibabu kama vile kutoa dawa za agizo la daktari au kutoa utambuzi wa ugonjwa au kusimamia na kuratibu huduma za afya kwa mtoa huduma wako wa afya mmoja au zaidi. Tunaweza kufichua PHI yako kwa madaktari, watoa huduma, maduka ya dawa, watoa huduma za macho, na watoa huduma wengine wa afya ili kusimamia na kuratibu huduma zako za afya au matibabu. **2. Kwa Malipo.** Tunaweza kutumia na kufichua PHI yako ili sisi na vitengo vingine husika au watoa huduma za afya tuweze kutoza na kupokea malipo kutoka kwako, kutoka kwa kampuni yako ya bima, au mhusika mwingine. Hii inaweza kujumuisha kufanya ukaguzi kuhusu ustahiki wa kupata bima na Medicaid ya jimbo, Medicare, au mipango mingine ya afya, kubaini hali ya usajili, na kutoa PHI kwa wahusika wanaotusaidia kutuma bili na kukusanya malipo yetu. **3. Kwa Shughuli za Kiafya.** Tunaweza kutumia na kufichua PHI yako kwa shughuli zetu za kiafya na shughuli za kiafya za vitengo vingine husika ambavyo una uhusiano nao au ulikuwa na uhusiano nao, kama vile usimamizi na kupanga mipango ya ndani na shughuli zinazoboresha na kupunguza gharama za huduma tunazokupa. **4. Kuwasiliana Nawe kuhusu Bidhaa na Huduma Zinazohusiana za Afya.** Tunaweza kutumia na kufichua PHI yako ili kuwasiliana nawe kuhusu afya yako na masuala husika, ikiwemo bidhaa na huduma zetu zinazohusiana za afya. Kwa mfano, tunaweza kutumia au kufichua PHI yako kuratibu miadi na kuweka vikumbusho, kukujulisha kuhusu bidhaa na huduma zetu, au kukushauri kuhusu kinga na matibabu mbadala yaliyopo, ikijumuisha yanayopatikana kupitia utafiti. **5. Kwa Watu Wanaohusika na Matibabu Yako au Kulipia Matibabu Hayo.** Tunaweza kufichua PHI yako kwa mwanafamilia, jamaa, rafiki, au mtu mwingine uliyeteua, anayehusika na matibabu yako au katika kulipia matibabu yako, mradi unakubaliana na ufumbuzi huu, ulikuwa na fursa ya kupinga ila hukufanya hivyo, au kulingana na hali iliyopo tutumie uamuzi wetu wa kitaaluma kubaini kwamba ufumbuzi huo unafaa. **6. Kama Inavyotakiwa Kisheria.** Tutafichua PHI yako tunapotakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria za serikali, jimbo, au za mitaa, amri ya mahakama au amri sawia na hiyo. **7. Kuzuia Tishio Kubwa kwa Afya au Usalama.** Tunaweza kutumia au kufichua PHI yako inapohitajika ili kuzuia au kupunguza tishio kubwa kwa afya au usalama wa mtu yeyote au umma. **8. Kwa Shughuli za Usimamizi wa Afya.** Tunaweza kufichua PHI kwa wakala wa usimamizi wa afya kwa shughuli zilizoidhinishwa au zinazohitajika na sheria kama vile ukaguzi, uchunguzi, na uidhinishaji wa leseni au shughuli zingine zinazohitajika kwa usimamizi wa mfumo wa huduma za afya, mipango ya faida, au haki za kiraia. **9. Kwa Afya na Usalama wa Umma.** Tunaweza kufichua PHI yako kwa mamlaka za serikali kwa ajili ya shughuli za afya na usalama wa umma kama vile kuzuia au kudhibiti ugonjwa, majeraha, au ulemavu, kuripoti unyanyasaji, utelekezaji, au unyanyasaji wa kinyumbani, na kuripoti urejeshaji wa dawa au madhara yanayotokana na dawa. **10. Kwa Kesi za Mahakamani na Kiutawala.** Tunaweza kufichua PHI yako wakati wa kesi ya mahakama au ya kiutawala kufuatia amri ya kisheria au mchakato mwingine wa kisheria. **11. Utekelezaji wa Sheria.** Tunaweza kufichua PHI kwa maafisa wa utekelezaji wa sheria kwa madhumuni fulani ya utekelezaji wa sheria, kama vile kuripoti uhalifu kwenye majengo yetu au kujibu maswali halali ya utekelezaji wa sheria. **12. Kwa Majukumu Maalum ya Serikali.** Tunaweza kufichua PHI yako: (1) ikiwa wewe ni mwanajeshi, kama inavyotakiwa na mamlaka ya kijeshi; (2) ikiwa wewe ni mfungwa au uko kizuizini, kwa idara ya magereza au afisa wa utekelezaji wa sheria; (3) kufuatia ombi kutoka kwa idara ya utekelezaji wa sheria, katika hali fulani; (4) kwa sababu za usalama wa kitaifa zilizoidhinishwa na sheria; (5) kwa maafisa wa serikali walioidhinishwa kumlinda Rais, watu wengine walioidhinishwa, au marais wa nchi za kigeni. **13. Kufidia Wafanyakazi.** Tunaweza kufichua PHI yako kulingana na sheria ya jimbo inayohusiana na fidia ya wafanyakazi au mipango mingine sawia. **14. Kwa Uchangiaji wa Viungo na Tishu.** Tunaweza kufichua PHI yako kwa ununuzi wa viungo au shughuli zingine sawia kwa madhumuni ya uchangiaji au upandikizaji. **15. Kwa Wachunguzi wa Vifo na Waelekezi wa Mazishi.** Tunaweza kufichua PHI kwa msimamizi wa machari, mchunguzi wa vifo, au mchunguzi wa kiafya kwa mujibu wa sheria husika ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao. **16. Kwa Wawakilishi wa Kibinafsi.** Tunaweza kufichua PHI yako kwa mtu aliyeidhinishwa kisheria kuchua hatua kwa niaba yako, kama vile mzazi, mlezi wa kisheria, au mtawala au msimamizi wa mali yako. **17. Kuthibitisha Umepokea Chanjo.** Tunaweza kutoa uthibitisho wa chanjo kwa shule kuhusu mwanafunzi au mwanafunzi mtarajiwa, kama inavyohitajika kisheria, ikiwa imeidhinishwa na mzazi/mlezi, mtoto aliyejisimamia kisheria, au mtu mwingine aliyeidhinishwa kama inavyohitajika. **18. Utafiti.** Tunaweza kutumia au kufichua PHI yako kwa madhumuni yafuatayo ya utafiti: (1) kulingana na ombi la kuondolewa la bodi ya ukaguzi ya kitaasisi au bodi inayosimamia masuala ya faragha; (2) kujiandaa kufanya utafiti; na (3) kama data mahususi (PHI ambapo maelezo mengi ya utambulisho yameondolewa). **19. Washirika wa Biashara.** Tunaweza kufichua PHI yako kwa Washirika wa Biashara ambao tunawapa kandarasi ya kutufanyia huduma fulani, kama vile huduma za malipo au usimamizi.

**Matumizi na Ufichuzi wa PHI Unaohitaji Idhini Yako:** Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa, hatutatumia wala kufichua PHI yako bila idhini yako au kama inavyoruhusiwa kisheria. Unaweza kuondoa idhini yako kwa kuandika ombi wakati wowote kama ilivyoagizwa kwenye idhini au kwa kuandikia HIPAA Compliance, 1 Customer Drive, Mailstop 0230, Bentonville, AR 72716. Ukiondoa idhini yako , tutasitisha matumizi au ufichuzi wa PHI kwa madhumuni yaliyowekwa kwenye idhini yako uliyotia saini, isipokuwa kwa kiwango ambacho tayari tumetumia idhini hiyo au kadri tulivyozuiwa kisheria. Sharti pia tuzingatie sheria husika ambayo ni kali zaidi kuliko HIPAA. **1. Kuuza PHI.** Hatuwezi kuuza PHI yako bila idhini yako iliyoandikwa au kama inavyoruhusiwa na HIPAA. **2. Madokezo kuhusu Matibabu ya Kisaikolojia.** Isipokuwa katika hali maalum, hatuwezi kutumia au kufichua maelezo ya matibabu ya kisaikolojia yaliyonakiliwa na mtaalamu wa afya ya kiakili akirekodi mazungumzo yako katika kipindi cha ushauri bila idhini yako. **3. Matangazo.** Sharti tupate idhini yako iliyoandikwa kabla ya kutumia au kufichua PHI yako kwa ajili ya matangazo. **4. Madhumuni ya Utafiti.** Kwa idhini yako, tunaweza kutumia au kufichua PHI yako kwa madhumuni mengine ya utafiti ambayo hayajaelezwa hapa juu.

**Rekodi za Mpango wa "Part 2":** Tunaweza kupokea PHI yako kutoka kwa mpango wa matumizi ya dawa za kulevya unaojumuisha maelezo chini ya 42 CFR Sehemu ya 2 ("Part 2") inayosimamia usiri wa rekodi za matumizi ya dawa za kulevya. Mpango wa "Part 2" una vidhibiti zaidi vya usiri vya rekodi za matumizi ya dawa za kulevya tunazopokea kupitia mpango wa "Part 2". Hatutatumia wala kufichua rekodi za matumizi ya dawa za kulevya tunazopokea kupitia mpango wa "part 2", au ushahidi unaohusiana na maudhui ya rekodi hizo, katika kesi za kiraia, za jinai, za kiutawala, au za kisheria dhidi yako isipokuwa kwa idhini yako iliyoandikwa au kufuatia amri ya mahakama baada ya kupokea notisi na baada ya wewe au mmiliki rekodi kupata fursa ya kujieleza. Amri ya mahakama inayoruhusu matumizi au ufichuzi sharti iwe na hati ya kuwasilisha kesi au mahitaji mengine ya kisheria ya kushurutisha ufichuzi kabla ya rekodi iliyoombwa kutumika au kufichuliwa.

**Una Haki Zifuatazo Kuhusiana na PHI Yako:** 1. Unaweza kuomba vizuizi kwa matumizi au ufichuaji wa PHI yako kwa matibabu, malipo au shughuli za utunzaji wa afya, au ufichuaji wetu wa PHI yako kwa mtu anayehusika katika utunzaji wako au malipo kwa utunzaji wako, kama vile mwanafamilia au rafiki. Hatuhitaji kukubali masharti haya. Tukikubaliana, tutatimiza ombi lako isipokuwa katika hali fulani za dharura au kama inavyotakiwa kisheria. 2. Unaweza kuomba vizuizi kwa ufichuaji fulani wa PHI yako kwa mpango wako wa afya kwa madhumuni ya kutekeleza matibabu, malipo au shughuli za utunzaji wa kiafya kuhusiana na huduma zilizolipiwa kikamilifu (kulipia mwenyewe). 3. Unaweza kukagua na kupokea nakala ya rekodi zako tulizohifadhi au unaweza kuagiza nakala hizo zishirikiwe na mtu uliyeteua. Katika hali fulani, tunaweza kukuzuia kufikia baadhi ya rekodi zako. Ukiomba nakala, huenda tukakutoza ada husika. 4. Unaweza kutuomba tubadilishe PHI fulani ikiwa si sahihi au haijakamilika. Sharti uwe na sababu ya kuunga mkono ombi lako. Tunaweza kukataa ombi lako ikiwa PHI ni sahihi na kamili, au sio sehemu ya PHI iliyohifadhiwa na au kwa mtoa huduma husika. Tukikataa ombi lako, una haki ya kuwasilisha taarifa ya kupinga hatua hiyo. Ombi lako litakuwa sehemu ya rekodi yako ya matibabu, itakayojumuishwa wakati tunapofanya ufichuzi wa kipengee au maelezo unayoamini kuwa hayajakamilika au si sahihi. 5. Unaweza kuomba taarifa kuhusu ufichuzi wa PHI yako. Hii ni orodha ya ufichuaji wa PHI yako, isipokuwa kwa madhumuni ya matibabu, malipo au shughuli za utunzaji wa kiafya, na hali zingine maalum zilizoruhusiwa kisheria. Ombi lako linapaswa kubainisha muda, usiozidi miaka sita kuanzia tarehe ya ombi. 6. Unaweza kutuomba tuwasiliane nawe kwa njia fulani au katika eneo fulani. Kwa mfano, unaweza kutuomba tuwasiliane nawe tu kazini au kwenye makazi au sanduku la posta tofauti. Ombi lako lililoandikwa linapaswa kuelezea ni jinsi gani au wapi unataka mawasiliano nawe. Tutakubali maombi yanayofaa. Ikiwa ungependa kutumia haki yako yoyote kati ya hizi, wasiliana na tawi la Walmart au la Sam's Club lililotoa huduma zako ili upate fomu husika, au andika ombi na uwasilishe kwa HIPAA Compliance, Walmart Inc., 2608 SE J Street, Mailstop 0230, Bentonville, AR. 72716. Unaweza kupata nakala iliyochapishwa ya Notisi hii kutoka tawi lako la Walmart, Sam's Club, au mtandaoni kupitia: https://corporate.walmart.com/privacy-security/notices.

**Huduma za Usaidizi za Lugha na Vifaa vya Usaidizi**: Chini ya kifungu cha 1557 cha Sheria ya Matibabu Nafuu, tunatoa huduma za usaidizi za lugha, vifaa vya na huduma za usaidizi bila malipo tunapopokea ombi kutoka kwa wateja, wahusika, wagonjwa, washiriki, wanufaika, waliosajiliwa, na wanaowasilisha maombi kupitia mipango, shughuli au huduma zetu za afya.

**Mabadiliko ya Notisi Hii:** Tuna haki ya kubadilisha Notisi hii na kutekeleza Notisi iliyofanyiwa marekebisho kuhusiana na PHI tunayodhibiti tayari au tutakayopokea baadaye. Tutachapisha nakala ya Notisi ya sasa. Tukibadilisha Notisi yetu, unaweza kupata nakala ya Notisi iliyofanyiwa marekebisho kwa kuwasilisha ombi au mtandaoni kupitia: https://corporate.walmart.com/privacy-security/notices.

**Kwa Maelezo Zaidi au Kuripoti Tatizo:** Ikiwa una swali kuhusu Notisi hii, wasiliana na HIPAA Compliance, Walmart Inc., 1 Customer Drive, Mailstop 0230, Bentonville, AR. 72716, au piga simu (800) WAL-MART. Ikiwa unaamini haki zako za faragha zimekiukwa, unaweza kuandika na kuwasilisha malalamishi, na hutachukuliwa hatua kwa hilo, kwa Afisa wa Kufuata Sheria wa HIPAA kupitia anwani iliyo hapa juu, au kwa Katibu wa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu, Ofisi ya Haki za Kiraia.

**Changanua Msimbo wa QR ili upate nakala za kidijitali za notisi hizi pamoja na Notisi zingine za Afya na Siha**